

TAARIFA KWA WAOMBAJI WA KAZI**Tafadhali fuata hatua zifuatazo wakati wa kuomba kazi:****HATUA 1: UJAZAJI WA FOMU ZA MAOMBI YA KAZI na MAOMBI KUPITIA BARUA PEPE**

Maombi Kupitia Serikali Za Mitaa: Tafadhali jaza fomu ya maombi ya kazi ya Yapi Merkezi iliyopo ofisi za serikali za mtaa. Fomu za maombi ya kazi husambazwa na Yapi Merkezi kwenye ofisi za serikali za mitaa kipindi ambacho mradi unahitaji nguvu kazi. (Hii inamaanisha kwamba kwenye baadhi ya nyakati fomu za maombi ya kazi huenda zisipatikane kwenye ofisi za serikali za mitaa).

Ufikishaji wa Fomu za Maombi ya Kazi: Kumbuka kuandika jina lako kamili kwenye fomu kama lilivyoandikwa kwenye kitambulisho chako. Utakapomaliza kujaza fomu tafadhali ifikishe kwenye serikali yako ya mtaa. Karani wa Yapi Merkezi (YM-OAC) atazikusanya fomu za maombi ya kazi kwa ajili ya tathmini zaidi.

Maombi Kupitia e-mail: Pia maombi ya kazi yanaweza kutumwa kupitia email; oac@ym.com.tr na muombaji aandike kazi anayoomba na jina lake kamili kwenye sehemu ya kichwa cha habari cha email na juu ya CV yake.

To: oac@ym.com.tr
Cc:
Subject: Jina Kamili (Nafasi Unayoomba)

To: oac@ym.com.tr
Cc:
Subject: Abdullah Mhandi (Dumptruck Driver)

Mambo Muhimu Ya Kuzingatia: WASIFU (CV) ni lazima uoneshe nafasi ya kazi unayoiomba, namba sahihi ya simu ya mkononi, tarehe ya kuzaliwa, mahali unapoishi, kiwango chako cha elimu, pamoja na uzoefu wako wa kazi. Waombaji wanashauriwa kutumia namba za simu zilizosajiriwa kwa majina yao.

Kama hauna WASIFU (CV): Tafadhali andika nafasi ya kazi unayoiomba na jina lako kamili kwenye sehemu ya kichwa cha habari cha barua pepe (email) yako (angalia mfano kwenye picha kushoto). Hakikisha unaandika namba yako ya simu pamoja na mahali unapoishi.

Viambatanisho: Tafadhali **USIAMBATANISHE** barua, cheti au kitambulisho chochote kile kwenye barua pepe (email). Nyaraka hizi zitahitajika baada ya tathmini ya awali ya ombi lako. Pia usitume tovuti (link) kwa ajili ya WASIFU (CV) wako; unaweza kuambatanisha nyaraka halisi ya WASIFU (CV) wako tuu.

HATUA 2: MCHUJO WA USAILI

Waombaji waliopitishwa kwenye mchujo wa awamu ya kwanza wataalikwa kwa kupigiwa simu na kupewa ratiba (tarehe, muda na siku) ya usaili. Orodha ya majina ya wasailiwa yatabandikwa kwenye ubao wa matangazo wa kituo cha tathmini ya ajira. Waombaji wa kazi watatakiwa kuhakiki taarifa zao kwa kuangalia taarifa zao kwenye ubao wa matangazo ili kuepuka udanganyifu.

HATUA 3: USAILI

Wasailiwa wote wanatakiwa kuja na kitambulisho halali katika kituo cha tathmini ya ajira kwa muda na tarehe sahihi kama ulivyoarifiwa kwenye simu. Maombi ya kazi yanaweza kukataliwa endapo msailiwa asipokuwa na kitambulisho sahihi au kushindwa kufika kwenye usaili ndani ya muda na tarehe iliyopangwa.

HATUA 4: MATOKEO YA USAILI

Utajulishwa matokeo ya usaili na tathmini kwa kupigiwa simu. Wasailiwa waliofaulu watatakiwa kuchukua vipimo vya afya pamoja na kukusanya nyaraka nyingine za ajira kwa ajili ya kuwekwa kwenye kanzidata (watu wanaosubiri uhitaji wa idara husika ili waitwe kuanza kazi).

MUHIMU:

- **Fomu ya maombi haiuzwi.** Fomu za maombi ya kazi zilizotolewa nakala(kopi) zitakataliwa, Hivyo basi epuka kununua nakala (kopi) au fomu bandia kutoka kwa **wahalifu/wadanganyifu/matapeli**.
- Watahniwa wataalikwa kwa **kupigiwa simu** na majina kubandikwa katika **ubao wa matangazo** katika kituo cha usaili kwa kufuata mtiririko kama ilivyopokelewa kutoka ofisi za serikali za mtaa. Tafadhali kuwa mvumilivu ukisubiri kupangiwa siku ya kufanyiwa tathmini kwa kuwa tuna idadi kubwa ya maombi tunayoyafanyia kazi.
- **Yapi Merkezi** haishirikiani na kampuni zozote za kuajiri au mtu yoyote katika kutoa ajira. **Yapi Merkezi** haitozi gharama yoyote kwa wanaotuma maombi au kuomba kazi. Hivyo kuwa muangalifu/makini na matapeli wanaoweza kukuahidi kukupa nafasi au kipaumbele kwenye usaili, ajira au kuharakisha mchakato wa kuajiriwa.
- **YAPI MERKEZI** inaajiri kutegemeana na uhitaji wa mradi. Kutuma maombi ya kazi na kufuzu usaili/tathmini hakukuhakikishii kupata ajira.
- Tafadhali kuwa na subira, na usisubiri nje ya geti la ofisi yetu ya usaili kama bado haujapewa taarifa zozote za matokeo ya usaili kwa kupigiwa simu na mfanyakazi wa kituo cha tathmini ya ajira.

JIHADHARI NA USISHAWISHIKE NA AJIRA ZISIZO HALALI NA PIA FIKISHA UJUMBE KWA WENGINE!